OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

HOTUBA YAMWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI – MHE. HAMZA S. JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI UFUNGUZI WA MKUTANO WA PILI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 UKUMBI WA LUSH GARDEN, JIJINI ARUSHA TAREHE 27 APRILI, 2026

- **Bw. Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Faith Minani, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu;**
- **Bw. Rashid Kigalu, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Dorina Kalumuna, Katibu wa TUGHE, Tawi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Mwakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi,**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana;**

Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi; Wageni Waalikwa; Waandishi wa Habari, Mabibi na Mabwana.

Kazi na Utu……!

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ……!

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, afya na fursa ya kukutana siku ya leo katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vile vile natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kadhalika, ninawashukuru wajumbe wa Baraza, wageni waalikwa kwa kutenga muda wenu ili kuungana nasi katika siku hii. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila, nisipowashukuru wajumbe wa Sekretarieti na wote waliohusika kwa namna mbalimbali kuandaa Mkutano huu. Ninatambua kuwa, mnayo majukumu mazito, lakini kwa kutambua umuhimu wa mkutano huu, mmeacha shughuli zenu ili mjumuike katika shughuli hii. Hongereni sana.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Kama mnavyofahamu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa chini ya Ibara ya 59 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikiwa na jukumu la kuishauri Serikali kuhusu mambo yote ya kisheria, ndani na nje ya nchi. Ofisi inatekeleza majukumu hayo kupitia Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 pamoja na sheria mbalimbali za kazi, kama vile, Agizo la Rais Na. 1 la mwaka 1970, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2003, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 na Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105.

Kwa mujibu wa sheria hizo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ilivyo kwa Taasisi zingine za Umma, inapaswa kuwashirikisha wafanyakazi wake katika masuala mbalimbali yanayohusu maslahi yao, ikiwemo kuandaa

na kutekeleza mpango na bajeti na kujadili hoja mbalimbali zinazotokana na utekelezaji wa mpango na bajeti ili kuzishauri menejimenti ipasavyo. Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 13.1 (c) ya Mkataba uliounda Baraza la Wafanyakazi kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na TUGHE wa mwaka 2020, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapaswa kufanya Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi si chini ya mara mbili kwa mwaka. Napenda kuwafahamisha kwamba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza takwa hili kikamilifu.

Ndugu wajumbe wa Baraza,

Baraza la wafanyakazi ni jukwaa muhimu mahala pa kazi. Baraza, mbali na kuwa kiunganishi kati ya Menejimenti na Wafanyakazi pia ni chombo cha ushauri na usimamizi katika kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, na wanazingatia maadili ya utumishi wao ili kuhakikisha tija katika utendaji.

Vilevile, DIRA YA TAIFA 2050 inalenga kuwa na Utumishi wa umma unaowajibika. Matarajio ni kuwa na Utumishi wa Umma unaofanya kazi kwa ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na wenye kupambana na rushwa. Ili kufanikisha hayo yote kwa ngazi ya taasisi ni lazima kuwa na ushirikishwaji wa watumishi katika utekelezaji wa majukumu na ufanyaji maamuzi. Ni dhahiri kuwa, Mabaraza ya wafanyakazi ni nyenzo muhimu kwa ustawi wa watumishi, taasisi na Taifa katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

“Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Baraza hili ni sauti yetu moja”

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Kama ambavyo sote tunafahamu, moja kati ya ajenda ya mkutano huu ni kuwawezesha wafanyakazi kupitia makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa **2026/27** kwa kuzingatia Ukomo wa Bajeti, Malengo ya

Taasisi na Maeneo ya Vipaumbele. Utaratibu huu unalenga kukuza uwazi na ushirikishwaji katika maamuzi mbalimbali ya taasisi ili mtumishi anapotekeleza majukumu yake atambue matarajio ya Dira na Dhima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwake. Vilevile, mtumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapaswa kufahamu bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli zake ndani ya Taasisi na mipango mbalimbali ya taasisi iliyopo kwa mwaka husika. Kwa hiyo, mtumishi atafanya kazi kwa kuzingatia malengo yaliyobainishwa pamoja na rasilimali zilizokadiriwa kutumika katika kufikiwa malengo hayo.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Niwasihi tukajadili agenda hii kwa weledi. Hakikisheni kuwa malengo na vipaumbele tulivyojiwekea kama taasisi, vinalenga kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za kisheria na kuboresha ustawi wa watumishi kulingana na bajeti ya Ofisi ya mwaka 2026/27.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Katika mwaka huu wa fedha, Ofisi yetu imepanga kutumia jumla ya Shilingi **Bilioni 61,091,334,000/=**. Kati ya pesa hizo, Shilingi **Bilioni 4,809,900,000/=** ni kwa ajili ya mishahara (PE) wakati Shilingi **Bilioni 52,281,434,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na Shilingi **Bilioni 4,000,000,000/=** ni kwa ajili ya maendeleo ya ndani. Bajeti inaonyesha ongezeko la takribani asilimia **49%** ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita. Ongezeko hili ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, katika kuimarisha sekta ya sheria nchini hususan kuiongezea uwezo Ofisi katika kutekeleza jukumu la kuishauri Serikali.

Niwasihi wajumbe wote wa Baraza kuitumia bajeti hii kwa tija, weledi na uadilifu mkubwa. Hakikisheni kuwa, kila shilingi inayotumiwa inaleta matokeo chanya katika kulinda, kuhifadhi na kudumisha rasilimali na maslahi ya nchi.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Nitumie fursa hii kuishukuru kwa dhati Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa jinsi inavyoendelea kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuipatia rasilimali na vitendea kazi mbalimbali. Ongezeko la bajeti lililobainishwa punde, ambalo linafikia jumla ya Shilingi **Bilioni 20.149,380,000/=** kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, ni ishara ya wazi kuwa Mheshimiwa Rais anatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Ofisi hii. Kwa hiyo tunapaswa kuhakikisha kuwa, jitihada zetu katika maeneo na ngazi mbalimbali zinaakisi uwekezaji huo mkubwa wa kifedha katika utekelezaji wetu wa majukumu mbalimbali.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Mara ya mwisho tulipokutana katika Baraza hili, mlibainisha changamoto kadhaa ikiwemo; uduni wa maslahi, upungufu wa motisha kazini, ukosefu au uhaba wa vitendea kazi muhimu ikiwemo magari, kompyuta mpakato, upungufu wa watumishi, ukosefu wa mafunzo kazini, ukosefu au uhaba wa fursa za ushiriki katika shughuli za michezo, na kadhalika. Ni furaha yangu kusikia leo hii mkitoa shukrani kwa namna Serikali yetu ilivyojitahidi kuzitatua changamoto husika kwa kiasi kikubwa.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Katika Risala ya Chama ca Wafanyakazi wa Serikali, Tawi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeelezwa vyema kwamba mengi yamefanyika katika kipindi kifupi. Kwa kuyataja, baadhi ya hayo ni:

i. Kuboreshwa kwa kiasi kikubwa kwa mazingira ya kazi;
ii. Jumla ya watumishi wapya 15 wameajiriwa na watumishi 24 wamepokelewa kwa njia ya uhamisho;

iii. Jumla ya watumishi 199 wamepatiwa mafunzo nje na ndani ya nchi,
iv. Kifurushi maalum cha nyongeza cha NHIF kimelipiwa na kinawanufaisha watumishi wote;
v. Maslahi ya watumishi yameboreshwa;
vi. Ofisi za mikoa zimepatiwa magari na kuongezewa watumishi;
vii. Vitendea kazi, ikiwemo magari na kompyuta mpakato vimenunuliwa;
viii. Taratibu za kufungua Ofisi tisa za mikoa zimekamilika na wakati wowote zitafunguliwa; na
ix. Ushiriki wa watumishi katika shughuli za michezo umeimarishwa.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Nimepokea na kusikiliza kwa umakini maombi yaliyowasilishwa katika Risala ya Chama cha wafanyakazi, Tawi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baadhi ya mambo hayo ni:

i. Mpango wa mafunzo ya muda mfupi uwe wazi na uwiainishwe na bajeti ya kila mwaka;
ii. Maboresho ya mishahara;
iii. Kuwepo kwa bajeti ya kutosha kwenye Sikukuu ya Mei Mosi ili Viongozi wa Taasisi na Halmashauri ya Tawi kushiriki;
iv. Kuwekwa wazi kwa malipo ya stahiki za watumishi wanaokuwa masomoni kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi;
v. Kutolewa ufafanuzi wa kiwango cha posho za kujikimu kwa watumishi kwa Mujibu wa Waraka wa Posho, ili kuondoa changamoto ya watumishi kulipwa kiwango cha posho kinachofanana sawa bila kuzingatia vyeo;
vi. Ofisi imshike mkono kwa “Asante ya Mwajiri”, Mtumishi anapostaafu utumishi wa umma katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

vii. Taarifa kwamba, Mawakili walioanzia kazi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hawatapanda madaraja; na

viii. Uwepo wa utaratibu wa utoaji rambirambi nje ya pesa ambazo watumishi wanakatwa kwenye mshahara unawaumiza watumishi.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Naomba kuwahakikishia kuwa, maombi yenu yote yamepokelewa; yatachakatwa kwa umakini, yatazingatiwa na kuyafanyiwa kazi. Kama tumeweza kutekeleza yaliyoonekana makubwa, hayo hayatatushinda. Na kwa yale yanayohitaji ufafanuzi au kujengewa uelewa, mtafafanuliwa, jitihada kuwezesha hayo zitafanyika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo. Endeleeni kuchapa kazi kwa kasi, mkijitoa kweli kweli.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Niwasihi yafuatayo;

i. Tujiepushe kabisa na desturi ya kufanya kazi kwa mazoea; Kila mmoja akawajibike kikamilifu katika nafasi yake;

ii. Endeleeni kudumisha maelewano, kuvumiliana, ushirikiano, umoja, upendo, amani na utulivu katika mazingira ya kazi; wakati wote mkajiepushe na matendo yanayokiuka maadili ikiwemo matumizi mabaya ya madaraka, uzembe, uvivu, migogoro pamoja na migongano isiyo na tija mahala pa kazi ili kuepuka hatari ya kuchafua taswira ya Ofisi na Serikali;

iii. Katunzeni siri za Ofisi wakati wote;

iv. Hakikisheni kuwa, daima uhusiano kati ya Menejimenti, Watumishi na Chama cha Wafanyakazi (TUGHE) unaongozwa na misingi ya kutegemeana, ushirikiano, utu, umoja, kuaminiana, kuthaminiana na kuheshimiana wakati wote. Kunapotokea kutofautiana katika mitazamo au maamuzi, mhakikishe tofauti hizo zinamalizwa kwa njia ya majadiliano ya pamoja, kwa kuongozwa na nia njema, taarifa sahihi na kamili, uhalisia na mantiki badala ya hisia tu. Tufanye hivyo

tukitambua kuwa, katika zama za sasa, njia ya mazungumzo ndiyo msingi mkuu wa mabaraza ya wafanyakazi bora duniani kote. Kwa kuzingatia hilo, ndiyo tutaweza kulinda maslahi mapana ya Ofisi yetu na Taifa kwa ujumla.

Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Kwa kuhitimisha, ni matumaini yangu kuwa mtalitumia Baraza hili kuhimizana kuhusu umuhimu wa kila mtumishi kutambua wajibu alio nao, pamoja na mambo mengine, katika kutumia vyema muda wa kazi kwa kutekeleza majukumu yake kwa bidii na weledi, ili kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria, kupitia utoaji wa huduma za kisheria kwa ubora unaotakiwa na ufanisi na tija inayotarajiwa kwa wadau mbalimbali. Naamini katika kikao hiki, mtatoka na maamuzi yatakayoiwezesha Ofisi hii kusonga mbele zaidi. Kwa kutambua kuwa, *“ Penye wengi hapaharibiki neno,”* basi Baraza ni mahali pa mashauriano na maelewano kwa faida ya wote.

Kwa kuwa kesho sote tutakutana hapa tena katika Mkutano wetu wa watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kwa kuwa nyinyi nyote mtakuwepo, mniruhusu kuhitimisha kwa haya machache. Kesho tutazungumza mengi na kwa kina.

Baada ya kusema haya, sasa natamka rasmi kuwa **Mkutano wa Pili wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, umefunguliwa rasmi.**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali …….. !

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.